



TAASISI YA TEKNOLOJIA DAR ES SALAAM

MAHAFALI YA KUMI NA MOJA YA TAASISI

Mkuu wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) anawatangazia wahitimu na wadau wote wa DIT kuwa Mahafali ya Kumi na Moja (11) ya Taasisi yamepangwa kufanyika Jumamosi, tarehe **16 Desemba, 2017**.

Mahafali haya yatatanguliwa na siku ya utoaji tuzo kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo yao katika mwaka wa masomo 2016/2017, sherehe ambazo zitafanyika Ijumaa, tarehe **15 Desemba, 2017**.

Taasisi inapenda kuwataarifu wahitimu wa Shahada ya Uzamili (M.Eng) na Shahada ya Kwanza (B.Eng/BTech), kusoma utaratibu na hatimaye kuthibitisha ushiriki wao katika Mahafali hayo kupitia tovuti ya Taasisi (www.dit.ac.tz)

Wahitimu watakaoshiriki wanapaswa kulipia joho la Mahafali **Tsh. 50,000/=** (kwa wahitimu wa Shahada ya Uzamili) na **Tsh. 30,000/=** (kwa wahitimu wa Shahada ya Kwanza katika tawi lolote la **NBC** kwenye akaunti namba **018101003145** na hatimaye kujisajili kupitia tovuti ya Taasisi (www.dit.ac.tz). *Watakaoruhusiwa kushiriki Mahafali haya ni wale tu watakaokamilisha usajili wao.*

ZINGATIA: Malipo yafanyike kwa kutumia jina kamili kama linavyoonekana kwenye orodha ya wahitimu wa mwaka 2016/17 iliyopo kwenye tovuti ya Taasisi, namba ya usajili na madhumuni ya malipo yaani Mahafali.

Kwa wanafunzi wa Stashahada (OD) ambao hawatavaa majoho wanatakiwa kuvaa nguo safi, nadhifu na zenye staha. Na hawa wanatakiwa kuthibitisha ushiriki wao kupitia tovuti ya Taasisi (www.dit.ac.tz) bila kulipia gharama zozote.

“Rehersal” itafanyika Alhamisi, tarehe **14 Desemba, 2017**.

Mwisho wa kujisajili ni tarehe **15 Novemba, 2017**.

Atakayeona tangazo hili anaombwa kumjulisha mwenzake.

Tangazo hili limetolewa na:

**Ofisi ya Uhusiano,
Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam,
S.L.P 2958,
Dar es Salaam.**